# MATAIFA YOTE.

Zaburi: Epifania

PETER AMMI
CUEA-Nairobi
06 Jan., 2023




1. Ee Mungu mpe mfalme hukumu zako, na mwana wa mfalme haki yako*
   Atawaamua watu wake kwa haki, na watu wako walioonewa kwa hukumu.

2. Siku zake yeye mtu mwenye haki atastawi, na wingi wa amani hata mwezi utakapokoma,*
   Na awe na enzi toka bahari hata bahari, toka mto hata miisho ya dunia.

3. Wafalme wa Tarshishi na visiwa walete kodi, wafalme wa Sheba na Seba na watoe vipawa*
   Naam, wafalme wote na wamsujudie, na mataifa yote wamtumikie.

.